HABARI KITAIFA

# Mpango atoa maagizo 8 taasisi za umma eGA

**Na Romana Mallya,** ARUSHA



MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango ametoa maagizo manane kwa taasisi za umma, ikiwamo kuzingatia sheria, kanuni, miongozo inayotolewa na mamlaka husika kutekeleza shughuli za serikali mtandaoni.

Amesema ni muhimu kulinda usalama wa mifumo na kudhibiti uhalifu wa kimtandao kwa kuendelea kushirikiana na vyombo vya dola na taasisi nyingine zinazohusika.

Dk. Mpango aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua Mkutano wa Tano wa Mamlaka ya Serikali Mtandao (eGA) unaofanyika kwa siku tatu.

Mkutano huo umebebwa na kaulimbiu: "Jitihada na ubunifu wa serikali mtandao kwa utoaji huduma za umma kwa ufanisi".

Amemwagiza Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora, George Simbachawene, mikoa miwili ambayo haijaingia katika mfumo wa E-Office, ifanye hivyo hadi Juni 30, mwaka huu.

"Pili, ni muhimu kituo cha utafiti kama ambavyo Bunge limeshauri, kiimarishwe na kuongezewa nafasi.

Kadhalika, kuhakikisha vipaumbele vya eGA vinasimamiwa ipasavyo na kusisitiza agizo ambalo mara kadhaa Rais Samia Suluhu Hassan, huliagiza la mifumo ya kusomana na kubadilisha taarifa.

Dk. Mpango aliagiza pia, suala la uzingatiaji wa sheria, kanuni, viwango na miongozo ya serikali mtandao katika uanzishaji na uendelezaji wa miradi yote ya TEHAMA serikalini.

Dk. Mpango alisema ripoti ya Benki ya Dunia (WB) ya mwaka 2022 inayojumuisha nchi 198 duniani kuhusu ukomavu wa matumizi ya teknolojia duniani katika utoaji wa huduma za serikali na ushirikishwaji wananchi ilibainisha Tanzania imefanya vizuri katika eneo hilo.

Kwa mujibu wa utafiti huo, Tanzania imepanda daraja kutoka kundi B hadi A na kushika nafasi ya 26 duniani na nafasi ya pili Afrika baada ya Mauritius na ya kwanza Afrika Mashariki.

Alisema mafanikio hayo yanatokana na utayari wa serikali kusimamia kwa usahihi matumizi ya TEHAMA katika taasisi zake, uwapo wa sera, sheria, miongozo na uwapo wa eGA.

**KUOMBA KUPUMZIKA**

Akimjibu Waziri Simbachawene kuhusu ombi lake kwa Rais kupumzika katika nafasi hiyo aliloliibua katika mkutano huo, Dk. Mpango alisema Sensa ya 2022 inaonesha takribani asilimia 77 ya watahiniwa kwa sasa ni vijana.

"Mimi nimetumika kwa muda mrefu na sasa mwezi Julai ninatimiza miaka 68. Chuo kikuu peke yake nimefundisha miaka 14, Benki ya Dunia miaka mitano nikijumlisha nikiwa msaidizi wa Rais Jakaya Kikwete, Ikulu, Naibu Katibu Hazina, Katibu Mtendaji Tume ya Mipango miaka sita,TRA mwezi mmoja, Wizara ya Fedha miaka mitano na miezi minne na sasa nafasi hii kubwa miaka mingine minne.Ninadhani inatosha," alisema.

Dk. Mpango alisema angependa kila inavyowezekana watumie muda kuandika, ili kuliachia taifa kumbukumbu nzuri kwa kuchangia historia ya mama Tanzania.

Awali, Simbachawene katika hotuba yake kwenye mkutano huo alisema kwa mshangao mkubwa walimsikia Rais akisema kuhusu uamuzi wa Dk. Mpango, ambao amedai wengine walisema ni mgonjwa.

Kuhusu eGA, Simbachawene alisema ina jukumu la kuboresha utendaji wa serikali katika kutoa huduma kwa wananchi, hivyo ni chombo kinachorahisha shughuli mbalimbali.

Mafanikio ya kujivunia ni, ujenzi wa mifumo mbalimbali ambayo imerahisisha serikali kuweza kuwa na urahisi wa utoaji huduma na kuwa na kasi. Hata majirani zetu wanakuja kujifunza kwetu," alisema.

Makamu Mwenyekiti Bodi ya Wakurugenzi Serikali Mtandao, Dk. Jasmine Tiisekwa, alisema mamlaka iko tayari kupokea maelekezo ili kujenga serikali.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka hiyo, Mhandisi Benedict Ndomba, alisema tangu kuanzishwa kwake mafanikio mbalimbali yamepatikana ikiwamo ujenzi wa mifumo mbalimbali iliyofanywa wazawa.

Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Ikulu, Mululi Mahendeka, alisema serikali mtandao ni nyenzo muhimu katika kuleta utawala bora na pia, kuongeza ufanisi serikalini na kurahisisha utoaji huduma bora.


**KUPOTEA KWA PASPOTI YA KUSAFIRIA**



**HAJI ZARIA SALUMU** anatangaza kupotea kwa passport ya kusafiria yenye namba **TAE 147099** iliyotolewa **DAR ES SALAAM PCO** Mei **23, 2019.** Kwa yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi kilicho karibu yake .

**TAARIFA POLISI : PHQ/DAR/KIN/21739/2025**


# Fundi friji asakwa madai kumlaghai mwenza wake kisha akamuua usiku

**Na Julieth Mkireri,** BAGAMOYO

JESHI la Polisi mkoani Pwani linamsaka Abdallah Mohamed (40) fundi friji, mkazi wa Mataya wilayani Bagamoyo kwa tuhuma za mauaji ya mzazi mwenzake, Naomi Mwakajengele (28).

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Salim Morcase, alisema jana kuwa amesema tukio hilo lilitokea usiku wa kuamkia Februari 10, mwaka huu, wakati Mohamed na Mwakajengele, mwalimu wa Shule ya Msingi Mataya, wakiwa chumbani kwao.



Kamanda Morcase alisema siku ya tukio usiku wa saa 8:00, zilisikika kelele kutoka kwa Mwakajengele akidai mwenza wake anamuua na baada ya muda mfupi, Mohamed alitoka ndani na kwenda chumba cha dada wa kazi.

Kwa mujibu wa Morcase, Mohamed alimtaka dada wa kazi kulala na watoto wa wawili mmoja wa miaka minne na mwingine miwili ambao awali walikuwa wamelalala na mama yao.

Alisema dada wa kazi alishtuka asubuhi pale jirani alipokuwa akimwita Mohamed huku mlango ukiwa wazi bila kufahamu kwamba aliondoka muda gani na kwenda kusikojulikana.

Kamanda alisema Mohamed aliondoka muda usiojulikana na haijajulikana aliko hadi jana baada ya tukio hilo.

Alisema uchunguzi wa awali umebaini kwamba mwili wa Mwakajengele ulichomwa na kitu chenye ncha kali ubavu wa kushoto, kulia na kwenye chembe ya moyo.

Pia alisema kabla ya tukio hilo, wawili hao walikuwa na tofauti zilizosababisha kutengana kwa muda mrefu kabla ya Mohamed kurudi wiki mbili zilizopita kabla ya kutokea mauaji hayo.


